**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA 04 CHA BODI YA WAMACU LTD KILICHOFANYIKA TAREHE 23/01/2023 KATIKA OFISI ZA WAMACU TARIME MJINI, KUANZIA SAA 09:30AM AHSUBUHI.**

- **Mahudhurio**

**WAJUMBE & KATIBU WA BODI YA WAMACU LTD**

1. David Mwita Hechei - M/kiti wa Bodi
2. Samwel Gisiboye Marwa - Katibu
3. Michael Joseph Mugwewa - M/M/Kiti
4. Elius Marwa Samwel - Mjumbe
5. Momanyi Range - Mjumbe

**WAJUMBE WAKARIBISHWA.**

6. James Marwa Makorom - Mwakilishi
7. Francis B. Chacha (Director MBL ) - Mwekezaji sheli ya mafuta

**WATENDAJI/SECRETARIET**

8. Mohamed Sakilu - Mhasibu Msaidizi
9. Bashiru R. namchambe - Mkaguzi wa Ndani Msaidizi
10. Olais Piniel Siray - Meneja Shughuli na Biashara

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

11. Kurwa Nyamohanga Mwita - Mjumbe
12. Julius Makonyo Makara - Mjumbe
13. Emmanuel Ndege Bensoni - Mjumbe

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Majadiliano ya bei na mwekezaji wa kituo kidogo cha mafuta(shell) katika eneo la WAMACU LTD;
3. Kujadili hoja za ukaguzi kwa mwaka 2021/2022; na
4. Kufunga kikao.

**AG.Na.01/4: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu wa kikao alisimama na kuwasalimia wajumbe wa kikao kwa salamu ya ushirika, na baada ya salamu aliendelea na utambulisho wa wajumbe wa kikao cha BODI. Pia aliwafahamisha wajumbe kuwa hiki ni kikao cha dharura cha 04 cha Bodi cha utekelezaji wa **AGENDA Na.05 na AZIMIO Na. 1 & 2** la kukubali uwekezaji wa kituo kidogo cha mafuta na la kumwita kwenye kikao

cha majadiliano cha tarehe 16/01/2023. Aidha katibu alisoma AGENDA mbele ya wajumbe na kuwafahamisha kuwa katika kikao hiki kutakuwa na AGENDA 2, na ya pili itakuwa ni kujibu hoja za ukaguzi kwa mwaka 2021/2022; baada ya kusema hayo katibu alimkaribisha M/kiti wa BODI **Ndg. David Hechei** kufungua kikao.

M/kiti Ndg. David Hechei, alisimama na kufungua kikao mnamo saa tatu (09:59am) ahsubuhi kwa kuwasalimia wajumbe na kabla ya kuanza AGENDA za kikao M/kiti ametoa taarifa ya safari ya Dodoma kuwa ulikuwa wito wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Taifa pamoja na kusisitiza juu ya dhumuni la kikao hicho kama ifuatavyo:-

1. Namna ya kupunguza Hati mbaya za ukaguzi;
2. Uchangiaji wa hisa katika Benki ya Taifa ya Ushirika NCBT; na
3. Namna tunavyoweza kupata hisa hizo katika ushirika.

Aidha M/kiti alifafanua aina ya hati mbalimbali zinazotolewa katika kikao cha Bodi, na kuwaeleza wajumbe juu ya umuhimu wa kuwa na hati safi. Pia alisisitiza kuwa ni lazma awepo Mkaguzi wa Ndani mwenye CPA ambaye atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa za chama zinakuwa katika misingi inayohitajika ili kuhakikisha tunaweka mpango wa utatuzi juu ya swala la dosari hizo.

Pia M/kiti alihimiza kuwepo kwa kamati mbalimbali za kusimamia shughuli ili kupunguza gharama za uendeshaji; Aliendelea kuwafahamisha wajumbe kuwa Vyama vyote vilivyopata Hati mbaya (chafu) vianaandaliwa barua ya kujieleza juu ya taarifa hizo na TCDC.

M/kiti baada ya kumaliza kutoa taarifa ya safari yake Dodoma alikaa na kusema kikao amekiweka huru kwa ajili ya kusomwa AGENDA inayofuta.

**AG.NA.02/4: MAJADILIANO YA BEI NA MWEKEZAJI WA KITUO KIDOGO CHA MAFUTA (SHELL) KATIKA ENEO LA WAMACU LTD**

Katibu alisoma AGENDA hii na kuwajulisha wajumbe kuwa sasa kinachohitajika ni majadiliano ya muda pamoja na bei ya uwekezaji yaani kodi kwa mwezi/mwaka kwa kila itakapokuwa inahitajika kufanya hivyo. M/kiti amehoji mwekezaji kuwa ni kwa namna gani atafanya uwekezaji wake wa biashara hiyo kwenye eneo hilo. **Ndg Mwangwa** amejitambulisha na kuonyesha namna atakavyofanya kazi, na atafanya kitu ambacho kitaleta ushindani ili tuweze kufanya taratibu zote za uwekezaji.

**Bwana Mwangwa,** amefafanua zaidi kuwa kazi hiyo itafanyika kwa uwazi pamoja na kushirikiana na wahandisi wa chama. Pia **M/kiti** alihoji juu ya idadi ya pumbu zitakazowekwa kwenye shell hiyo? Na Mjumbe Momanyi Range amesisitiza juu ya Ubora wa hali ya juu katika kuwekeza ili kupata kitu cha kudumu na kufanya makubaliano ambayo yatazingatia ubora wa hali ya juu.

**Bwana Mwangu** amesema kituo kizuri kinaenda hadi milioni mia tatu (300,000,000/=), pia amesema proposal yake ni ya bei nzuri ila tutajadiliana na kabla ya kujenga nitaleta ramani kwenye eneo kwa ajili ya kupitiwa upya.

**Ndg Makaro**m amehoji kuwa uwekezaji huu utakuwa wa muda gani kabla hatujaongea bei ya mwaka, akapewa majibu na **Bwana Mwangwa** kuwa mara nyingi huwa ni miaka 15, pia akaendelea kutoa mifano ya maeneo tofauti aliyowahi kujenga vituo vya Mafuta. Baada ya maelezo hayo ya muda wa uwekezaji; mjumbe Momanyi range alipendekeza bei ya kodi kwa mwaka kuwa iwe milioni 20.
**Bwana Mwangwa**, amejibu hoja vizuri kuwa ataanza na milioni 5 na kufanya mabadiliko ya kila mwaka; pia akatoa uzoefu wa biashara hii kuwa inapangwa na serikali hivyo chama kimfanyie milioni 5 kwa mwaka ila iwe inabadilika kila mwaka. Baada ya mvutano wa muda mrefu alikubali iwe milioni 6. Ndipo M/kiti akashauri kwa pamoja kuwa kukata mvutano huu alipendekeza bei iwe milioni 9. Hata hivyo baada ya kusema hivyo Ndg Mwangwa aliomba bei iwe milioni 8 ili tuache mvutano wa muda mrefu. Na wajumbe wote waliafiki kuwa bei iwe TZS milioni 8 kwa mwaka ila iwe inabadilika kila mwaka kadiri ya uchumi na gharama ya maisha inavyozidi kupanda. Baada ya mjadala wa muda mrefu maazimio yamewekwa kama ifuatavyo hapo chini.

**MAAZIMIO.**
1. Gharama ya kodi ya mwekezaji kwa mwaka itakuwa TZS milioni nane (8);
2. Muda wa kukoma kwa mwekezaji utakuwa ni miaka 15, na baada ya hapo yatafanyika majadiliano kwa ajili ya aidha kuendelea na upangaji au chama kuendelea na mradi wake;
3. Mkataba utasainiwa mara tu mwekezaji atakapokuwa ameweka fedha kwenye akaunti ya chama kwa mkupuo, kama malipo ya kodi ya miaka miwili au mwaka mmoja kadiri anavyoweza;
4. Gharama ya kodi itaendelea kubadilika kila mwaka kulingana na hali ya maisha ya kila siku na gharama za uchumi;
5. Mkataba ukisha saininiwa utapelekwa kwa Mrajisi kwa ajili ya kuidhinishwa kutumika.

**AG.NA.03/4: KUJADILI HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA 2021/2022.**
Katibu alisoma AGENDA hii ya hoja za ukaguzi kwa mwaka 2021/2022 na kuimba Bodi izijadili na kuondoa dosari zilizojitokeza kama hoja za ukaguzi kwa mwaka 2021/2022. Pia wajumbe walijaribu kuhoji swala la wadhamini kwa wafanyakazi na kila mtu alitoa maelezo yake na kujitetea kuwa wadhamini wao wapo watawaleta haraka iwezekanavyo. Pia wajumbe wa Bodi kwa pamoja waliekeza kuwa dosari zote zilizosababisha hoja za ukaguzi zifanyiwe kazi haraka sana na kurudishwa COASCO kwa ajili ya kufutwa ili tupewe Hati safi.

**MAAZIMIO.**

1. Katibu andae mikakati na utaratibu wa haraka wa kujibu hoja za ukaguzi ili dosari zote ziondolewe kwenye ripoti ndani ya siku saba kama ilivyo kisheria kwa ajili ya kupewa hati safi;
2. Bodi imetoa wiki moja kwa kila mtumishi kuleta mdhamini kwa ajili ya mkataba wake kusainiwa na kufailiwa; na
3. Na marekebisho haya yafanyike leo taarifa hii ya ukaguzi iende kufanyiwa kazi haraka irudi kusomwa kwenye Mkutano mkuu wa chama wa tarehe 27/01/2023;.
4. Utekelezaji huu ukikamilika usomwe kwenye kikao kijacho.

**AG.Na.04/4: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti Ndg. David Hehei, alisimama na kuwashukuru wajumbe wote wa BODI kwanza kwa kukubali kujadili AGENDA hizi mbili za kikao chadharura na kutoa michango yao iliyowezesha jambo hili kufanikiwa na hatimaye kupata mwekezaji wa kitu cha mafuta na kuondoa dosari za ukaguzi kwa ajili ya kurudishwa COASCO kwa marekebisho.

Pia aliwapongeza kwa uvumilivu na ushirikiano wao kwani kikao hiki kilikuwa cha dharura sana. Baada ya kusema hayo aliahirisha kikao mnamo saa 12:42 mchana na kuwatakia safari njema wajumbe waendapo majumbani mwao hadi hapo kikao kitakapoitishwa tena.

***Muhtasari huu umesainiwa kwa niaba ya wajumbe BODI na***

**..........................................** **..........................................**

**MWENYEKITI** **KATIBU**

TAREHE……………………………….